

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

**MUHTASASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE  
21/01/2022**

**KUMB.NA.CDC/UZ/12/2022 WALIOHUDHURIA**

## **A.WAJUMBE WALIOHUDHULIA**

NA	JINA	CHEO	
1	Bw.Cuthbert G.Mwinuka	Afisa kilimo	Mwenyekiti
2	Bibi .Salome P.Lyimo	Afisa Ugavi	Katibu
3	Bw.John F.Maholani	Afisa Utumishi	Mjumbe
4	Bw.Alex Batwel	Afisa Uchaguzi	Mjumbe
5	Dr.Darison Andrew	Kaimu Mganga Mkuu	Mjumbe

## **B:WAALIKWA**

**1.Bw Paul Mtua-Kaimu Mhandishi Ujenzi(W)**

## **C.SEKRETARIETI**

1	Bibi Sarah J Sompo	Mwandishi wa Vikao
---	--------------------	--------------------

## **KUMB.NA.CDC/UZ/13/2022 KUFUNGUA**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio yao.Akawataka kuwa makini,Kisha akafungua kikao saa 2:30 asubuhi

## **KUMBU.NA.CDC/UZ/14/2022 KUTHIBITISHA AJENDA**

Katibu aliwasilisha ajenda za kikao kama zinavyoonekana hapa chini

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda

3. Kupitia na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni tarehe 06/10/2021 na tarehe 03/01/2022
4. Kupitia taarifu ya tathmini jengo la dharula hospitali na nyumba ya watumishi 3 katika 1
5. Pendekezo la kujengo jengo la kutolea huduma za dharula(EMD)na nyumba ya watumishi 3 in 1 ,kituo cha afya Kambikatoto
6. Mengineyo
7. Kufunga kikao.

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuthibitisha agenda za kikao zilizokuwa mbele yao.Wajumbe walikubali kuwa ajenda hizo zijadiliwe

**KUMB.NA.CDC/UZ/14/2022 KUPITIA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI  
WA KIKAOCHA BODI YA ZABUNI TAREHE 06/10/2021 NA TAREHE  
03/01/2022**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kusoma na kupitia mihtasari ya vikao vya bodi ya zabuni vya tarehe 06/10/2021 na tarehe 03/01/2022,masahihisho ya uandishi wa wajumbe yalifanyika na kisha ikapitishwa kuwa kumbukumbu halali na ikathibitishwa.

**KUMB.NA.CDC/UZ/15/2022 KUPITIA TAARIFA YA TATHMINI JENGO LA  
DHARULA HOSPITALI NA NYUMBA YA WATUMISHI 3 KATIKA 1**

Katibu aliwasilisha taarifa ya tathmini ya jengo la dharula la hospitali na nyumba ya watumishi 3katika 1.Aidha ufanuzi ulitolewa kuwa kuna agizo la kutumia "Force Account" kujenga haya majengo.Wajumbe walipokea na kujadili kisha walishauri nyaraka ziwekwe zote kwani ajenda hii ya kupitia taarifa ya tathmini imeshafutwa kutokana na mabadiliko yaliyoletwa.

**KUMB.NA. CDC/UZ/22/2022 PENDEKEZO LA KUJENGA JENGO LA KUTOLEA HUDUMA ZA DHARULA (EMD) NA NYUMBA YA WATUMISHI 3 IN 1, KITUO CHA AFYA KAMBIKATOTO.**

Katibu aliwasilisha taarifa inayoitaka Halmashauri kujenga jengo la kutolea huduma za dharula (EMD) na nyumba ya watumishi 3 katika 1, kituo cha afya Kambikatoto kwa kutumia "Force Account", wajumbe waliipokea na kujadili kisha waliipitisha ila walishauri iwe makini.

**AZIMIO**

- Mhandisi aandae na alete BOQ tarehe 03 Januari asubuhi.
- Fursa za mawe, mchanga na kokoto zihamasishwe kutoka kwa wananchi

**KUMB.NA. CDC/UZ/23/2022 MENGINEYO**

Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti;

- Wajumbe walishauri kupata posho kwani hiki ni kikao cha bodi.
- Wajumbe waliomba pia hata uwezekano wa kubadilisha mazingira ya kufanya kikao ie.hotelini.

**KUMB.NA. CDC/UZ/24/2022 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa uvumilivu na ushiriki katika kikao na aliwatakitia utekelezaji mwema wa yaliyojadiliwa, kisha alifunga kikao mnamo saa 4:16 asubuhi.



BIBI. SALOME P. LYIMO  
KATIBU

UMETHIBITISHWA



BW. CUTHBERT G. MWINUKA

MWENYEKITI

10/02/2022  
TAREHE